# Matatizo ya Uchanganuzi wa Sentensi za Kiswahili kwa Wanafunzi wa Shule za Sekondari Nchini Tanzania

*Elishafati J. Ndumiwe*
*Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania (SAUT-Mwanza)*

**Ikisiri**

**Ufundishaji wa sintaksia katika vyuo vikuu nchini Tanzania unakabiliwa na matatizo ya kinadharia na kimaudhui (Kahigi na Hassan, 2020). Wahitimu wa vyuo vikuu hufanya kazi ya kufundisha wanafunzi wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari nchini Tanzania. Miongoni mwa mada zinazofundishwa katika somo la Kiswahili ni uchanganuzi wa sentensi. Matatizo ya kinadharia na kimaudhui wanayohitimu nayo walimu hao huvukizwa katika ufundishaji wa uchanganuzi wa sentensi. Kwa hiyo, makala haya yalichunguza matatizo ya uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania. Utafiti huu umefanyikia uwandani na maktabani. Mbinu iliyotumika kukusanya data za maktabani ni usomaji matini ilhali hojaji na jaribio zilitumika kukusanya data za uwandani. Data zilikusanywa kutoka shule 20 za sekondari nchini Tanzania (16 za bara na 4 za Zanzibar). Katika shule hizo, 10 zilikuwa za upili wa chini[1] na 10 za upili juu[2]. Mkabala wa kitaamuli ulitumika katika kuchambua data za utafiti huu. Data zilizokusanywa zilichanganuliwa kwa kuongozwa na Mkabala wa Kileksika ulioasisiwa na Lewis (1993). Matatizo yaliyobainika ni ugawanyaji wa mti-matawi katika matawi zaidi ya mawili, ukosefu wa maarifa kuhusu nadharia za uchanganuzi wa sentensi, dosari za uainishaji wa maneno, ubainishaji wa neno zaidi ya moja kama aina moja ya neno na uchanganyaji wa vipashio vya uchanganuzi. Baadhi ya vyanzo vya matatizo hayo ni dosari katika miongozo ya ufundishaji, vitabu na uhaba wa maarifa kwa waalimu wa sarufi katika shule za sekondari. Utafiti unapendekeza maboresho ya vitabu vya kiada na ziada, miongozo na mafunzo elekezi kwa waalimu wa sarufi katika shule za sekondari.**

**Maneno Muhimu:** *Uchanganuzi, Sentensi za Kiswahili, Sekondari, Upili wa Chini, Upili wa Juu*

## Utangulizi

Neno 'uchanganuzi' linatokana na kitenzi 'changanua'. Kwa mujibu wa TUKI (2013), kitenzi hiki kina fahiwa mbili. Fahiwa ya kwanza ni kutenganisha vitu vilivyoshikamana. Fahiwa ya pili ni kuchambua dhana, fikra au maandishi ya mtu. Makala haya yanaegemea katika fahiwa ya kwanza kwa sababu sentensi huundwa kwa vijenzi vidogovidogo viitwavyo maneno. Kwa hiyo, uchanganuzi wa sentensi ni utaratibu wa kubainisha na kutenganisha maneno yanayounda sentensi. Suala la uchanganuzi sentensi lilianzishwa na wanasarufi wa kale kama vile Plato (428-348 KK), Aristotle (384-322 KK), Socrates (469-399) na kundi la Stoiki kutoka Ugiriki. Magwiji hao walichanganua vipashio mbalimbali vilivyojitokeza katika lugha ya Kigiriki. Mathalani, Plato aligawa sentensi katika sehemu kuu mbili, yaani kiima na (kiarifu). Aristotle aliendeleza kazi ya mwalimu wake (Plato) kwa kuonesha maneno yanayounda sentensi, yaani nomino, kitenzi, kivumishi, kiunganishi na kielezi.

Wanasarufi wa mwanzoni wa lugha ya Kiswahili waliiga taratibu za uchanganuzi wa sentensi kutoka lugha hizo na kuziingiza katika sarufi ya lugha ya Kiswahili. Vitabu mbalimbali vya kiada na ziada viliandaliwa kwa lengo la kuwezesha ufundishaji wa sarufi ya lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari nchini Tanzania. Hata hivyo, Massamba, Kihore na Hokororo (2012) wanaeleza kuwa vitabu vya kiada na ziada vinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi katika shule za sekondari nchini Tanzania vina matatizo kadhaa. Vitabu vilivyorejelewa katika andiko hilo ni *Sarufi*

[1] Istilahi 'shule za upili wa chini' inarejelea elimu ya sekondari kidato cha I-IV

[2] Istilahi 'shule za upili wa juu' inarejelea elimu ya sekondari kidato cha V-VI

*na Fasihi katika Sekondari na Vyuo* kilichoandikwa na Nkwera (1978), *Kiswahili Sekondari* kilichotayarishwa na TET (1988) na *Sarufi Mpya* kilichoandikwa na Mohamed (1988). Matatizo yaliyobainishwa katika vitabu hivyo ni uchanganyaji wa mikabala (nadharia) ya uchanganuzi, matumizi ya istilahi tofautitofauti. Mathalani, baadhi ya waandishi wanatumia istilahi *fungu tenzi* huku wengine wakitumia istilahi *kikundi tenzi*. Vilevile, waandishi wengine hutumia istilahi *kirai kitenzi*.

Sanjari na vitabu hivyo, serikali ya Tanzania kupitia kwa wizara ya elimu na taasisi zake iliandaa miongozo kuhusu maudhui yanayopaswa kufundishwa kwa wanafunzi wa shule za upili wa chini na wa juu. Mihtasari inayotumika kufundisha somo la Kiswahili (uchanganuzi wa sentensi ukiwemo) iliandaliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi mwaka 2005 (kidato cha I-IV) na 2010 (kidato cha V-VI). Katika muhtasari wa Kiswahili ( kidato cha I-IV), uchanganuzi wa sentensi hufundishwa kidato cha tatu. Ndani ya muhtasari huo imelekezwa sentensi zichanganuliwe kwa njia ya majedwali na mchoroti (matawi) tu. Pia, katika muhtasari wa Kiswahili (kidato V-VI), uchanganuzi wa sentensi hufundishwa katika kidato cha sita. Ndani ya muhtasari huo imelekezwa sentensi zichanganuliwe kwa njia ya mchoroti (matawi), jedwali (visanduku), maelezo na mishale. Pamoja na mambo hayo, nadharia za uchanganuzi, hatua za uchanganuzi na aina za sentensi zinazochanganuliwa havijabainishwa. Kwa hiyo, uchanganuzi wa sentensi unakaofundishwa hutegemea maarifa, uwezo, uzoefu na rejea alizonazo mwalimu anayefundisha mada husika.

Walimu wanaofundisha mada ya uchanganuzi wa sentensi ni wale waliohitimu shahada ya awali katika elimu au stashahada katika elimu. Wahitimu hao huwa wameteua somo la Kiswahili kama mojawapo ya somo la kufundishia katika michepuo yao. Hata hivyo, Kahigi na Hassan (2020) wameeleza kuwa ufundishaji wa sintaksia ya Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Tanzania hukabiliwa na matatizo makuu mawili, yaani nadharia za kisintaksia au maarifa na stadi za kisintaksia ambazo mhitimu anapaswa kuwa nazo. Sambamba na matatizo hayo, kuna changamoto za uchanganyaji wa mikabala ya ufundishaji, uhaba wa wataalamu wa sintaksia ya Kiswahili na kukosekana kwa chombo cha kusimamia ufundishaji wa sintaksia ya Kiswahili katika vyuo vikuu na vyuo vya kati nchini Tanzania.Vilevile, Hassan (2021) anaeleza kuwa kuna uchanganyaji wa mikabala pamoja na istilahi zinazotumika katika ufindishaji wa sarufi ya Kiswahili katika elimu ya vyuo vikuu nchini Tanzania.

Kwa hiyo, walimu wanaofundisha mada ya uchanganuzi wa sentensi wana changamoto ya kinadharia na kimaudhui kuhusu sintaksia. Pia, rejea zinazotumika zina dosari lukuki na miongozo inayotumika haiko bayana kuhusu mada ya uchanganuzi wa sentensi. Makala haya yamechunguza matatizo waliyonayo wanafunzi katika kuchanganua sentensi za Kiswahili. Makala haya yamegawanyika katika sehemu saba. sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili ni kiunzi cha kinadharia. Methodolojia za utafiti zimeelezwa katika sehemu ya tatu. Sehemu ya nne ni matokeo ya utafiti. Sehemu ya tano inaeleza vyanzo vya matatizo ya uchanganuzi wa sentensi. Sehemu ya sita ni mapendekezo ya utafiti. Sehemu ya mwisho ni hitimisho la utafiti.

**Kiunzi cha Kinadharia**

Uchanganuzi wa data za makala haya umeongozwa na Mkabala wa Kileskika ulioasisiwa na Lewis (1993). Mkabala wa Kileksika ni mtazamo wa kisarufi unaoonesha kuwa sentensi huundwa kwa muunganiko wa viambajengo vidogovidogo. Kwa mujibu wa Lewis (1993), mkabala wa kileksika una misingi mitatu. Msingi wa kwanza ni mfuatano wa viambajengo vya kimuundo katika tungo. Kwa kuzingatia msingi huu, viambajengo vya kimuundo hushirikiana na viambajengo vingine katika kuzalisha tungo. Msingi wa pili ni uwakilishi wa kisintaksia katika muundo wa nje. Kuhusu msingi huu, uchanganuzi wa data kwa kutumia mkabala wa kileksika hautambui kuwapo kwa muundo wa ndani. Tungo huchanganuliwa kwa namna inavyojidhihirisha katika usemaji wa lugha husika. Msingi wa tatu ni uchanganuzi wa viambajengo vya tungo katika mchoroti, yaani mti-matawi. Kwa kuzingatia msingi huu, mkabala wa kileksika hushughulikia uchanganuzi wa viambajengo vya kimuundo katika mti-matawi.

Pamoja na kuwapo kwa misingi hiyo, uchanganuzi wa data za utafiti huu umetumia msingi wa kwanza na wa pili. Kwa kuzingatia misingi hii, mtafiti alichunguza sentensi zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya jaribio. Sentensi hizo zilichunguzwa kwa namna zilivyochanganuliwa katika data

iliyotolewa na watoaataarifa. Vilevile, mtafiti alichunguza namna viambajengo vilivyochanganuliwa kwa kuzingatia mfuatano wake katika uchanganuzi. Kwa hiyo, mkabala huu ulisaidia katika kubaini makosa ya kiuchanganuzi yanayofanywa na wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania.

**Methodolojia ya Utafiti**

Utafiti huu ulifanyikia uwandani na maktabani. Kwa upande wa maktabani, mtafiti alitumia mbinu ya usomaji matini kukusanya data za utafiti huu. Matini zilizoteuliwa ni muhtasari wa Kiswahili kwa elimu ya sekondari kidato cha I-IV, muhtasari wa Kiswahili kwa elimu ya sekondari kidato cha V-VI, vitabu vya Kiswahili kidato cha tatu na cha sita. Data za uwandani zilikusanywa kwa kutumia hojaji na jaribio la uchanganuzi wa sentensi. Data zilikusanywa kutoka shule 20 za sekondari nchini Tanzania (16 za bara na 4 za Zanzibar). Shule ziliteuliwa kinasibu ili kuwakilisha shule zingine kwa sababu utafiti usingeweza kufika shule zote kulingana na muda tuliokuwa nao na gharama ya kukamilisha kazi hiyo. Katika shule hizo, shule 10 zilikuwa za upili wa chini na 10 za upili juu. Watoataarifa 30 waliteuliwa katika utafiti huu. Katika kila shule, watoataarifa watatu (mwalimu mmoja na wanafunzi wawili) waliteuliwa. Watoataarifa hao waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji nasibu sahili. Watoataarifa walioteuliwa waliwakilisha watoataarifa wengine katika shule zilizoteuliwa. Jedwali Na.1 linaonesha msambao wa shule zilizoteuliwa katika utafiti huu:

**Jedwali Na. 1: Msambao wa Shule Zilizoteuliwa Kimikoa**

| **Mkoa** | **Idadi ya Shule za Sekondari** | | **Watoataarifa** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Upili wa Chini** | **Upili wa Juu** | | **Walimu** | **Wanafunzi** |
| Mwanza | 01 | 01 | | 01 | 02 |
| Rukwa | 01 | 01 | | 01 | 02 |
| Mbeya | 01 | 01 | | 01 | 02 |
| Singida | 01 | 01 | | 01 | 02 |
| Dodoma | 01 | 01 | | 01 | 02 |
| Mara | 01 | 01 | | 01 | 02 |
| Ruvuma | 01 | 01 | | 01 | 02 |
| Moshi | 01 | 01 | | 01 | 02 |
| Kaskazini Pemba | 01 | 01 | | 01 | 02 |
| Mjini Magharibi | 01 | 01 | | 01 | 02 |
| **Jumla ndogo** | 10 | 10 | | 10 | 20 |
| **Jumla Kuu** | 20 | | | 30 | |

**Chanzo:** Mtafiti (2021)

Data zilizokusanywa ziliwasilishwa kwa kutumia maelezo na vielelezo. Aidha, uchambuzi wa data ulitumia mkabala wa kitaamuli. Mbinu ya uchambuzi wa data kimuundo ilitumika katika kuchambua data zilizokusanywa. Kwa kuzingatia mbinu hii, mtafiti alichambua data zilizokusanywa kwa kuangalia muundo wa vielelezo vya mchoroti, jedwali, mishale au maelezo. Kupitia mbinu hii, mtafiti alibaini matatizo ya kiuchanganuzi wa sentensi yanayofanywa na wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania.


**Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu unaonesha kuwapo kwa matatizo kadhaa ya uchanganuzi wa sentensi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania. Matokeo haya yalibainika kupitia jaribio la uchanganuzi wa sentensi walilopewa wanafunzi. Sentensi sahili, changamani na ambatani zilijaribiwa kupima maarifa ya uchanganuzi wa sentensi. Aidha, sentensi hizo zilichanganuliwa kwa njia iliyoteuliwa na mwanafunzi mwenyewe. Matatizo yaliyobainika yameelezwa na kujadiliwa katika sehemu zinazofuata.

***Ugawanyaji wa Mti-Matawi katika Matawi zaidi ya Mawili***

Kwa mujibu wa Kayne (1994), mti-matawi (pia, huitwa ngoe au mchoroti) wa kiuchanganuzi unapaswa kugawika katika matawi mawili. Hata hivyo, wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania (upili wa chini na wa juu) hugawa viambajengo (hasa virai) vinavyojenga sentensi katika matawi zaidi ya mawili wakati wa uchanganuzi wa sentensi. Ugawanyaji huo huweza kukiuka miundo ya vijenzi vya kirai husika. Kwa kawaida, kirai hujengwa na neno kuu pamoja na kijalizo chake. Kwa msingi huo, mti-matawi unapaswa kuonesha vijenzi hivyo viwili, yaani neno kuu na kijalizo chake. Pia, kijalizo cha neno kuu kinaweza kuendelea kugawanywa kiuwili hadi kufikia kiambajengo cha mwisho zaidi. Kielelezo Na. 1 kinaonesha mfano wa uchanganuzi kutoka kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania. Uchanganuzi huo unadhihirisha sentensi ya, 'Juma ni mwalimu aliyetufundisha vizuri kucheza ngoma'.

**Kielelezo Na. 1: Ugawanyaji wa Mti-Matawi Zaidi ya Matawi Mawili**





**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)

Kiarifu (A) katika Kielelezo Na. 1 kimegawanywa katika matawi sita wakati wa uchanganuzi wa sentensi. Ugawanyaji huu unakiuka kanuni ya mgawanyo kiuwili iliyopendekezwa na Kayne (1994). Ugawanyaji wa namna hii huweza kuongeza makosa mengine ya uchanganuzi wa sentensi kama vile ukiukaji wa muundo wa virai na uainishaji wa maneno katika sentensi.

***Uchanganyaji wa Mikabala (Nadharia) za Kiuchanganuzi***

Baadhi ya vitabu vya kiada vimeonesha kuwa kuna mikabala (nadharia) miwili ya uchanganuzi wa sentensi, yaani kimapokeo na kimuundo. Hata hivyo, wanafunzi wengi katika shule za upili wa chini na wa juu nchini Tanzania wanachanganya mikabala hii wakati wa uchanganuzi wa sentensi. Wanafunzi hao huanza kuonesha kuwa sentensi inaundwa na kiima (K) na kiarifu (A). Kisha, huonesha kuwa kiima huundwa na kirai nomino (KN) na kiarifu huundwa na kirai kitenzi (KT). Kimsingi, ubainishaji wa kiima na kiarifu hudokeza kuwa uchanganuzi umeongozwa na mkabala wa kimapokeo ilhali KN na KT huonesha kuwa uchanganuzi umeongozwa na mkabala wa kimuundo. Kwa hiyo, matumizi ya istilahi hizo huonesha uchanganyaji wa mikabala ya uchanganuzi wa sentensi. Kielelezo Na. 2 kinaonesha mfano wa uchanganyaji wa mikabala kwa wanafunzi wa shule za sekondari chini Tanzania katika uchanganuzi wa sentensi, 'siku za mwizi ni arobaini':


**Kielelezo Na. 2: Uchanganyaji wa Mikabala ya Kiuchanganuzi katika Njia ya Matawi**




**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)

Kielelezo Na. 2 kinaonesha namna mwanafunzi alivyochanganya mikabala ya kiuchanganuzi. Katika ngazi ya pili ya mti-matawi, kuna kiima na kiarifu ilhali katika ngazi ya tatu, kuna KN, KT na KE. Uchanganyaji wa namna hii hujitokeza pia katika njia zingine za uchanganuzi wa sentensi. Utafiti huu umebaini kuwa katika njia ya maelezo, wanafunzi huchanganya mkabala wa kimuundo na kimapokeo katika wa uchanganuzi wa sentensi. Kielelezo Na. 3 kinadhihirisha haya uchanganuzi wa sentensi, 'huyu ana haraka lakini yule anapenda kutulia':

**Kielelezo Na. 3: Uchanganyaji wa Mikabala ya Kiuchanganuzi katika Njia ya Maelezo**


Njia ya Maneno
Hii ni sentensi ambatano
Sentensi hii imeundwa na sentensi mbili
Sentensi ya kwanza imeundwa na kiima pamoja na kiarifu
Kiima kimeundwa na kirai nomino
Kirai nomino kimeundwa na kiwakilishi
Kiwakilishi ni huyu.
Kiarifu kimeundwa na kirai kitenzi
Kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi pamoja na kielezi
Kitenzi ni Ana
Kielezi ni Haraka
Kirai kiunganishi kimeundwa na kiunganishi
Kiunganishi ni lakini


**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)

Katika Kielelezo Na. 3, kuna matumizi ya maneno 'kiima kimeundwa na kirai nomino' na 'kiarifu kimeundwa na kirai kitenzi'. Vipashio 'kiima na kiarifu' hutumika katika uchanganuzi wa sentensi kwa kuzingatia mkabala wa kimapokeo. Aidha, vipashio 'kirai nomino na kirai kitenzi' hutumika katika uchanganuzi wa sentensi kwa kuzingatia mkabala wa kimuundo. Kwa hiyo, matumizi ya vipashio hivyo kwa pamoja huonesha kuwa wanafunzi wa shule za sekondari wanachanganya mikabala ya kiuchanganuzi katika uchanganuzi wao wa sentensi.

***Uchanganyaji wa Vipashio vya Kiuchanganuzi***

Vipashio vinavyotumika wakati wa uchanganuzi wa sentensi sharti viendane na mkabala wa uchanganuzi unaotumika (Hassan, 2021). Mikabala tofautitofauti inapotumika sambamba wakati wa uchanganuzi husababisha vipashio vya uchanganuzi kuchanganywa. Utafiti huu umebaini kuwa wanafunzi wengi wanapotumia mkabala wa kimuundo hutumia pia vipashio vya kiuamilifu (kidhima), kama vile chagizo na shamirisho wakati huohuo. Vilevile, wanapotumia mkabala wa kimapokeo hutumia vipashio vya kimuundo, kama vile KN, KV, KT au KE. Uchanganyaji huo unashindwa kuweka mipaka ya matumizi ya vipashio katika uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili. Kielelezo Na. 3 kinaonesha uchanganyaji wa vipashio vya kimuundo katika uchanganuzi wa sentensi kimapokeo kwa kurejelea sentensi, 'shangazi alikuwa anasoma kitabu polepole':

**Kielelezo Na. 4: Uchanganyaji wa Vipashio vya Kimuundo katika Uchanganuzi wa Kimapokeo**





**Chanzo:** Data ya Utafiti

Vipashio 'kiima (K)', kiarifu (A), 'shamirisho (Sh)' na 'chagizo (Ch)' katika Kielelezo Na. 4 ni vipashio vya kimapokeo. Hata hivyo, vipashio 'kirai nomino (KN)', kirai kitenzo (KT), 'kitenzi kisaidizi (Ts)' na 'kitenzi kikuu (T)' katika kielelezo hicho ni vipashio vya kimuundo. Kwa hiyo, wanafunzi wengi huchanganya vipashio vya kimuundo na vya kimapokeo wakati wa uchanganuzi wa sentensi.

Sambamba na hilo, wanafunzi wengine huchanganya vipashio vya kimapokeo katika uchanganuzi wa kimuundo. Sentensi huchanganuliwa kwa kuonyeshwa kuwa huundwa na kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT). Baada ya ubainishaji huo, vipashio vya kimapokeo hubainishwa kama mojawapo ya vijenzi vya kirai kitenzi. Mara nyingi, vipashio vinavyochanganywa huwa ni shamirisho, chagizo au prediketa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.5.

**Kielelezo Na. 5: Uchanganyaji wa Vipashio vya Kimapokeo katika Uchanganuzi wa Kimuundo**





**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)

Kielelezo Na. 5 kinaonesha matumizi ya vipashio vya kimapokeo 'shamirisho' na 'chagizo' katika uchanganuzi wa kimuundo. Vipashio hivyo vimebainishwa kama vijenzi mojawapo vya kirai kitenzi (KT). Tatizo hili huchagizwa na kuwapo kwa mikabala tofautitofauti ya kiuchanganuzi katika ngazi moja ya elimu. Kwa hiyo, ufundishaji wa mikabala yote husababisha wanafunzi waichanganye wakati wa uchanganuzi wa sentensi.

***Ubainishaji wa Kifungu cha Maneno kama Neno Moja***

Uchanganuzi wa sentensi hufikia tamati kwa kubainisha kategoria za kileksika zinazounda sentensi inayochanganuliwa. Kila neno lililopo katika sentensi hupaswa kubainishwa kwa kuoneshwa aina ya neno hilo. Kimsingi, neno katika maandishi hubainika kirahisi kwa sababu hutenganishwa na nafasi kila upande. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa baadhi ya vifungu vya maneno huainishwa kama neno moja, yaani kategoria moja ya kileksika. Uainishaji unaofanyika huzingatia kategoria ya neno mojawapo katika kifungu husika. Katika Kielelezo Na. 6, wanafunzi alibainisha kirai nomino 'kalamu na daftari' kama neno moja katika sentensi, nipatie kalamu na daftari':

**Kielelezo Na. 6: Ubainishaji na Uainishaji wa Kirai Nomino kama Nomino**





**Chanzo:** Data za Utafiti (2021)

Kielelezo Na. 6 kinaonesha uchanganuzi ulifanyika kwa kubainisha kirai nomino 'kalamu na daftari' kama nomino. Kimsingi, uchanganuzi ungeliweza kuendelea kwa kuonesha vijenzi tofautitofauti vinavyojenga kirai nomino 'kalamu na daftari. vijenzi hivyo ni kirai kiunganishi na kirai nomino kingine.

Pia, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kirai kitenzi huweza kubainishwa na kuainishwa kama neno moja. Uainishaji unaofanyika huzingatia kijenzi mojawapo cha kirai kitenzi katika sentensi husika. Katika mfano uliotolewa, mwanafunzi alibainisha kirai kitenzi 'ana haraka' na anapenda kulia, kama chagizo kinachoundwa na kielezi. Kielelezo Na. 7 kinadhihirisha haya kupitia uchanganuzi wa sentensi, huyu ana haraka lakini yule anapenda kutulia':

**Kielelezo Na. 7: Ubainishaji na Uainishaji wa Kirai Kitenzi kama Chagizo**





**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)

Kirai kitenzi 'ana haraka' na 'anapenda kulia' katika Kielelezo Na. 7 kimebainishwa na kuainishwa kama neno moja ambalo ni chagizo (kielezi). Hata hivyo, virai hivyo vimeandikwa kwa kuachanishwa nafasi. Suala hili huonesha kuwa ni maneno mawili yanayojitegemea. Zaidi ya hayo, uchanganuzi wa sentensi hiyo una makosa lukuki. Pamoja na uchanganuzi kudokeza kuwa sentensi tajwa ni sentensi ambatani lakini hakuna vitenzi vilivyobainishwa katika uainishaji huo.

***Makosa ya Uainishaji wa Maneno katika Sentensi***

Uainishaji wa maneno katika sentensi huzingatia mofolojia ya neno husika au dhima ya neno hilo katika sentensi (Ndumiwe, 2022). Kwa kuzingatia mofolojia ya neno, neno huainishwa kutegemeana na umbo lake. Aidha, dhima ya neno huzingatia utokeaji pamoja na maneno mengine katika sentensi. Pamoja na kuwapo kwa vigezo hivyo, utafiti huu umebaini kuwa yapo makosa mengi ya uainishaji wa maneno katika sentensi zinazochanganuliwa na wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania. Aina za maneno zinazoainishwa ni tofauti na uhalisia wake kulingana na mfuatano wa maneno mengine katika sentensi. Kwa mfano, kihusishi kimeainishwa kwa namna tatu tofautitofauti na wanafunzi. Namna ya kwanza, kimeainishwa kama kiunganishi. Namna ya pili, kimeainishwa kama kama kivumishi. Namna ya mwisho kimeainishwa kama kitenzi. Kielelezo Na. 8-10 kinadhihirisha maelezo haya kupitia uchanganuzi wa sentensi, 'siku za mwizi ni arobaini':

**Kielelezo Na. 8: Uainishaji wa Kihusishi kama Kiunganishi**





**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)

Kielelezo Na. 8 kinaonesha kihusishi ‘za’ kimeainishwa kama kiunganishi. Kimsingi, kiunganishi huunganisha neno na neno, kirai na kirai, kishazi na kishazi au sentensi na sentensi. Mazingira yaliyopo katika Kielelezo Na. 8 ni neno na neno (nomino). Hata hivyo, dhima ya neno ‘za’ katika Kielelezo Na. 8 siyo kuunganisha bali kuonesha uhusiano wa nomino ‘siku’ na nomino’mwizi’. Sambamba na makosa hayo, kuna makosa pia ya kuainisha neno ‘mwizi’ kama chagizo badala ya nomino. Vilevile, neno ‘ni’ limeainishwa kama kivumishi badala ya kitenzi kishirikishi.

Aidha, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa neno ‘za’ limeainishwa kama kivumishi badala ya kihusishi. Kimsingi, kivumishi ni neno lenye uamilifu wa kutoa sifa kuhusu nomino au kiwakilishi. Kivumishi hutokea baada ya nomino, kibainishi au kiwakilishi. Neno ‘za’ katika Kielelezo Na. 9 hutokea baada ya nomino ‘siku’. Hata hivyo, haina dhima ya kutoa sifa kwa nomino iliyotangulia badala yake inaonesha uhusiano wa nomino ‘siku’ na ‘mwizi’. Kielelezo Na. 9 kinadhihirisha haya.

**Kielelezo Na. 9: Uainishaji wa Kihusishi kama Kivumishi**





**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)

Katika Kielelezo Na. 9, neno ‘za’ limeainishwa kama kivumishi badala ya kihusishi. Sambamba na hilo, neno ‘arobaini’ limeainishwa kama kielezi badala ya nomino. Makosa haya yanatokana na wanafunzi kukariri kuwa kivumishi tu ndicho hutokea baada ya nomino na kielezi hutokea baada ya kitenzi.

Sanjari na hayo, matokeo yanaonesha kuwa neno ‘za’ huainishwa kama kitenzi kikuu badala ya kihusishi. Kwa msingi huo, neno ‘za’ hutokea katika upande wa kirai kitenzi wala siyo upande wa kirai nomino. Kielelezo Na. 10 kinaonesha uainishaji wa neno ‘za’ kama kitenzi kikuu badala ya kihusishi.

**Kielelezo Na. 10: Uainishaji wa Kihusishi kama Kitenzi**




**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)


Katika Kielelezo Na. 10, neno ‘za’ limeainishwa kama kitenzi kikuu badala ya kihusishi. Neno hilo limetokea baada ya nomino ‘siku’. Mazingira haya huweza kutokea aina tofautitofauti za maneno kama vile kihusishi, kibainishi, kitenzi, kivumishi au kiunganishi. Uwezekano wa kutokea kwa aina hizo huchochea mkanganyiko wa uainishaji wa neno ‘za’ kama kitenzi badala ya kihusishi. Sambamba na makosa hayo, uchanganuzi unaonesha kuwa sentensi ina kitenzi kikuu na kitenzi

kishirikishi kwa pamoja. Kwa kawaida, sentensi sahili za Kiswahili haziwezi kuundwa na kitenzi kikuu na kitenzi kishirikishi kwa pamoja.

***Ukiushi wa Muundo wa Virai, Kiima au Kiarifu***

Virai katika lugha ya Kiswahili huundwa kwa neno moja au zaidi (Kihore na wenzake, 2012). Kirai kinapoundwa na zaidi ya neno moja hupangiliwa kwa utaratibu maalumu. Kiima nacho hujengwa na vipashio vinavyokaa pamoja kwa utaratibu maalumu. Vilevile, kiarifu hujengwa na kitenzi pamoja na maneno yanayotokea baada ya kitenzi. Matokeo yanaonesha kuwa ugawanyaji wa virai, kiima au kiarifu hukiuka muundo wa viambajengo hivyo katika lugha ya Kiswahili. Viambajengo visivyohusika katika muundo huo huwekwa pamoja kama sehemu ya vijenzi vya muundo huo. Kielelezo Na. 11 kinaonesha ukiukaji wa muundo wa kiarifu katika uchanganuzi wa kimatawi unaowakilisha sentensi, ‘siku za mwizi ni arobaini’:

**Kielelezo Na. 11: Ukiushi wa Muundo wa Kiima na Kiarifu katika Matawi**





**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)

Kielelezo Na. 11 kinaonesha kuwa kiarifu kimeundwa na kitenzi ‘za’, shamirisho ‘mwizi’, kitenzi kishirikishi ‘ni’ na kielezi ‘arobaini’. Ugawanyaji wa kiima na kiarifu kwa kuzingatia vipashio hivyo una makosa lukuki. Uchanganuzi uliopo katika kiarifu unaonesha kuwa kiarifu kina vitenzi viwili ndani yake, yaani kitenzi kishirikishi na kitenzi kikuu. Vitenzi hivyo hawiwezi kutokea pamoja katika sentensi za Kiswahili.

Vilevile, uchanganuzi uliopo katika Kielelezo Na. 12 unaonesha ukiushi wa muundo wa kiima na kiarifu. Katika uchanganuzi huo, kiima kinaundwa na kivumishi ilhali kiarifu kinaundwa na nomino, kiunganishi na nomino. Kwa kawaida, kiima sharti kiwe na nomino (dhahiri au kapa) au kiwakilishi ndani yake. Kiarifu sharti kiwe na prediketa ndani yake. Kielelezo Na. 12 kinadhihirisha haya katika uchanganuzi wa sentensi, ‘nipatie kalamu na daftari’:

**Kielelezo Na. 12: Ukiushi wa Muundo wa Kiima na Kiarifu katika Njia ya Jedwali**





**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)

Katika Kielelezo Na. 12, kiima kinaundwa na KV. Pia, kiarifu kinaundwa na KN+KU+KN. Miundo hii (ya kiima na kiarifu) imekiukwa kwa sababu kiima sharti kiwe na nomino au kiwakishi ndani yake. Vilevile, kiarifu sharti kiwe na kitenzi kikuu au kitenzi kishirikishi ndani yake.

Pia, katika Kielelezo Na. 13 ugawanyaji uliofanyika unakiuka muundo wa kirai kitenzi. Katika uchanganuzi huo, chagizo katika $S_1$ na $S_2$ imebainishwa kama kijenzi cha moja kwa moja kutoka katika $S_1$ na $S_2$ wala siyo kijenzi kilichopo chini ya KT. Kielelezo Na. 13 kinaonesha uchanganuzi wa sentensi, wazee waliondoka juzi lakini watoto wao wameondoka leo':

**Kielelezo Na. 13: Ukiushi wa Muundo wa Kirai Kitenzi kwa Njia ya Matawi.**





**Chanzo:** Data ya Utafiti (2021)

Kielelezo Na. 13 kinaonesha baadhi ya makosa ya ugawanyaji wa kirai kitenzi katika uchanganuzi wa wanafunzi wa shule za sekondari. Katika ugawanyaji huo, muundo wa kirai kitenzi umekiukwa kwa kuonesha chagizo kama kijenzi mojawapo cha darajia ya juu katika $S_1$ na $S_2$ badala ya kuwa kijenzi cha kirai kitenzi. Pamoja na dosari hiyo, kuna dosari ya uchanganyaji wa vipashio vya kiuchanganuzi.

***Makosa ya Ubainishaji wa Kirai Kiwakilishi***

Katika sarufi ya lugha ya Kiswahili, kiwakilishi ni muundo mmojawapo wa kirai nomino (Ndumiwe, 2020). Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari hubainisha kirai kiwakilishi (KW) kama mojawapo ya aina za kirai katika lugha ya Kiswahili. Utafiti uliofanyika ulibaini kuwa wanafunzi wengi hudhani kwamba kila aina ya neno inaunda kirai chake. Suala hili siyo sahihi kwa sababu aina za maneno zinazounda virai ni saba. Aina hizo ni nomino (kirai nomino), kitenzi (kirai kitenzi), kivumishi (kirai kivumishi), kibainishi (kirai kibainishi), kielezi (kirai kielezi), kihusishi (kirai kihusishi) na kiunganishi (kirai kiunganishi) (Matinde, 2012 na Ndumiwe, 2020). Kwa hiyo, ni makosa kubainisha kirai kiwakilishi kama mojawapo ya kirai cha Kiswahili. Kielelezo Na. 14 kinaonesha utokeaji wa kirai kiwakilishi katika uchanganuzi wa sentensi, huyu ana haraka lakini yule anapenda kutulia':

**Kielelezo Na. 14: Ubainishaji wa Kirai Kiwakilishi katika Uchanganuzi wa Sentensi**




**Chanzo:** Data ya Utafiti (2022)

Katika Kielelezo Na. 14, kuna kifupisho 'KW' kinachowakilisha kirai kiwakilishi. Chini yake ndipo kumebainishwa neno 'huyu' na 'yule' kama viambajengo tamati vya kifupisho hicho. Utambuzi

wa kirai kiwakilishi unaonesha kuwa uchanganuzi wa sentensi katika shule za sekondari bado una dosari lufufu.

***Vyanzo vya Matatizo ya Kiuchanganuzi kwa Wanafunzi wa Sekondari za Tanzania***

Katika utafiti huu, mtafiti alikusanya taarifa kutoka kwa walimu wa shule za sekondari na kupitia nyaraka mbalimbali, ikiwemo vitabu vya kufundishia na mihtasari ya somo la Kiswahili kwa shule za upili wa chini na wa juu. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa makosa ya kiuchanganuzi kwa wanafunzi wa sekondari nchini Tanzania yanasababishwa na mambo kadhaa. Mambo hayo ni ufiche wa miongozo ya ufundishaji, rejea zinazotumika kufundishia na changamoto za kimaudhui kutoka kwa walimu.


*Ufiche wa Miongozo ya Ufundishaji*

Miongozo (mihtasari) inayotumika kufundishia somo la Kiswahili katika shule za sekondari haijaweka wazi baadhi ya mambo muhimu katika uchanganuzi wa sentensi. Kwa mfano, muhtasari wa Kiswahili (kidato cha I-IV na cha V-VI) hakujaweka wazi aina za sentensi zinazopaswa kuchanganuliwa katika ngazi hizo. Vilevile, mkabala (nadharia) inayoongoza uchanganuzi wa sentensi katika ngazi hizo havijawekwa wazi. Ufiche huo hutengeneza ombwe kwa walimu wa ngazi hizo kufundisha yale wanayoweza au yale waliyofundishwa wakati wa mafunzo yao. Aidha, walimu wengine hufundisha yale wanayokutana nayo kwenye vitabu vya rejea wanavyovitumia. Kwa hiyo, ufiche wa miongozo ya ufundishaji ni chanzo kimojawapo cha matatizo ya uchanganuzi wa sentensi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania.

*Rejea za Ufundishaji*

Ufundishaji wa mada ya uchanganuzi wa sentensi hutumia vitabu vya kiada na ziada. Vitabu vya kiada huidhinishwa na wizara inayohusika na elimu au taaisisi za wizara hiyo kutumika katika ngazi husika ya elimu. Aidha, vitabu vya ziada hutumiwa na mwalimu kwa ajili ya kuongeza maarifa ya mada inayofundishwa. Kwa upande wa shule za upili wa chini, kitabu cha '*Kiswahili Kidato cha Tatu: Kitabu cha Mwanafunzi*' (John, 2011) na '*Kiswahili Shule za Sekondari: Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tatu*' (TET, 2021) vimeidhinishwa na wizara kutumika katika shule za upili wa chini. Hata hivyo, vitabu hivyo vya kiada bado vina dosari kuhusu uchanganuzi wa sentensi. Mathalani, ugawanyaji wa mti-matawi zaidi ya matawi mawili. Vilevile, kuna makosa ya uainishaji wa maneno katika sentensi.


**Kielelezo Na. 15: Mfano wa Uchanganuzi wa Sentensi kutoka TET (2021) na John (2011)**




**Chanzo**: John (2011:25) **Chanzo**: TET (2021:44)

Pia, kuna utofauti wa istilahi zinazotumika katika uchanganuzi katika vitabu tajwa. Mathalani, katika kitabu cha John (2019) istilahi 'T' (kitenzi kikuu) ilhali katika TET (2021), istilahi 'P' (prediketa) zinatumika katika uchanganuzi wa kimapokeo. Kadhalika, katika kitabu cha John (2011) istilahi 'KTg' (kishazi kitegemezi-vumishi) ilhali katika TET (2021) istilahi 'βv' (kishazi kitegemezi-vumishi) zinatumika katika uchanganuzi wa kimapokeo.

**Kielelezo Na. 16: Utofauti wa Kiistilahi katika John (2011) na TET (2021)**




**Chanzo:** John (2011:25) **Chanzo:** TET (2021:45)

Kielelezo Na. 16 kinaonesha utofauti unaojitokeza katika matumizi ya istilahi katika vitabu viwili vya Kiswahili vinavyotumika katika shule za sekondani nchini Tanzania. Kimsingi, istilahi 'βv' hutumika katika uchanganuzi wa kimapoke ilhali katika uchanganuzi wa kimuundo istilahi 'S' (sentensi) hutumika kuonesha sentensi iliyoshushwa hadhi na kukunjiwa katika KN. Aidha, istilahi 'P' (prediketa) hutumika katika uchanganuzi wa kimapokeo ilhali 'T' (kitenzi kikuu) hutumika katika uchanganuzi wa kimuundo. Kwa hiyo, dosari zilizopo katika rejea hizo husababisha matatizo kwa wanafunzi wakati wa kujifunza uchanganuzi wa sentensi.

Kwa upande wa shule za upili wa juu, kitabu cha John na Mduda (2012) *Kiswahili Kidato cha Tano na Sita* kimeidhinishwa kuwa kitabu cha kiada katika ngazi hiyo. Hata hivyo, zipo baadhi ya changamoto za kiuchanganuzi zinazijitokeza katika kitabu hicho. Miongoni mwa changamoto hizo ni matumizi ya istilahi zenye hadhi tofauti katika uchanganuzi wa mwelekeo mmoja. Kwa mfano, katika uchanganuzi wa kimapokeo, waandishi wameonesha kuwa kitenzi kisaidizi ni kijenzi mojawapo cha kishazi tegemezi vumishi. Kishazi tegemezi vumishi ni kipashio cha kidhima ilhali kitenzi kisaidizi ni kipashio cha kimuundo. Kielelezo Na. 17 kinaonesha mfano wa uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya maelezo kutoka kwa John na Mduda (2012).

**Kielelezo Na. 17: Uchanganyaji wa Istilahi za Kimuundo na Kidhima katika Maelezo**

*Mfano:* Mtoto wake aliyesafiri amesharudi.

Hii ni sentensi changamano.

Sentensi hii ina kiima na kiarifu.

Kiima kina jina, kivumishi na kishazi tegemezi kivumishi.

Jina ni "mtoto".

Kivumishi ni "wake".

Kishazi tegemezi kivumishi kina kitenzi kisaidizi.

Kitenzi kisaidizi ni "aliyesafiri".

Kiarifu kina kitenzi kikuu.

Kitenzi kikuu ni "amesharudi".

**Chanzo:** John na Mduda (2012:89)

Istilahi kitenzi kikuu, kivumishi na kitenzi kisaidizi katika Kielelezo Na. 17 ni za kimuundo ambazo zimechanganywa katika uchanganuzi wa kimapokeo. Uchanganuzi huo hupaswa kutumia istilahi za kdhima na wala siyo za kimuundo.

Vilevile, uchanganuzi katika mkabala wa kimuundo uliofanywa na John na Mduda (2012) kwa njia ya maelezo unachaganya istilahi za kidhima katika uchanganuzi wa kimuundo. Istilahi za

kidhima zilizotumika ni kishazi tegemezi kivumishi na shamirisho. Kielelezo Na. 18 kinadhihirisha haya.

**Kielelezo Na. 18: Uchanganyaji wa Istilahi za Kidhima katika Uchanganuzi wa Kimuundo**


*Mfano:* Mvua iliyonyesha imeezua mapaa mengi.
Hii ni sentensi changamano.
Sentensi hii ina kirai nomino na kirai tenzi.
Kirai nomino kina nomino na kishazi tegemezi kivumishi.
Nomino ni "Mvua".
Kishazi tegemezi kivumishi ni "iliyonyesha".
Kirai tenzi kina kitenzi kikuu na shamirisho.
Kitenzi kikuu ni "imeezua".
Shamirisho lina nomino na kivumishi.
Nomino ni "mapaa".
Kivumishi ni "mengi".

**Chanzo:** John na Mduda (2012:89)

Katika Kielelezo Na. 18, kuna istilahi za kidhima 'shamirisho' na 'kishazi tegemezi vumishi' katika uchanganuzi wa kimuundo. Kimsingi, uchanganuzi wa kimuundo hupaswa kutumia istilahi za kimuundo wala na wala siyo za kidhima.

Sanjari na hayo, katika vitabu vya ziada vinavyotumika katika shule za upili wa juu vina changamoto kadhaa kuhusu uchanganuzi wa sentensi. Kwa mfano, kitabu cha *Nadharia ya Lugha-Kiswahili 1: Kidato cha 5 na 6* (Masebo na Nyangwine, 2016) kina dosari kadhaa za uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili. Mathalani, ubainishaji wa kiambajengo zaidi ya kimoja kama kiambajengo kimoja. Kielelezo Na. 19 kinadhihirisha haya.

**Kielelezo Na. 19: Ubainishaji wa Kishazi kama Kivumishi katika Masebo na Nyangwine (2016:324)**





**Chanzo:** Masebo na Nyangwine (2016:324)

Katika kielelezo Na. 19, tunaona kiambajengo 'aliyekuletea maji ya kunywa' kikibainishwa kama kivumishi. Ubainishaji wa kiambajengo 'aliyekuletea maji ya kunywa' katika fundo tamati ni dosari kwa sababu sentensi hupaswa kuchanganuliwa kwa kuishia katika mafundo tamati ambayo hujengwa na neno mojamoja. Aidha, uainishaji wa kiambajengo 'aliyekuletea maji ya kunywa' kama kivumishi ni dosari kwa sababu kivumishi kina dhima ya kutoa sifa kuhusu nomino au kiwakilishi.

Pia, mifano ya uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya maelezo unaonesha uchanganyaji wa mikabala ya kiuchanganuzi. Katika uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya maelezo, waandishi wameonesha sentensi inaundwa na kiima na kiarifu; kisha, kiima kinaundwa na kirai kitenzi. Aidha, kiarifu kinaundwa na kirai kitenzi. Kielelezo Na. 20 kutoka kwa Masebo na Nyangwine (2016) kinadhihirisha haya:

**Kielelezo Na. 20: Uchanganyaji wa Mikabala ya Kiuchanganuzi katika Masebo na Nyangwine (2016:326)**




4. Maneno au maelezo
Kiswahili kinaweza kufundishia masomo yote shuleni.
Hii ni sentensi sahili
Sentensi ina kiima na kiarifu
Kiima kina nomino
Nomino ni "Kiswahili"
Kiarifu kuna kitenzi kisaidizi, kikuu, shamirisho na chagizo
Kitenzi kisaidizi ni "kinaweza"
Kitenzi kikuu ni "kufundishia"
Shamirisho ina nomino na kivumishi
Nomino ni "masomo"
Kivumishi ni "yote"
Chagizo kina kielezi
Kielezi ni "shuleni"

**Chanzo:** Masebo na Nyangwine (2016:326)

Istilahi 'kiima', kiarifu' katika Kielelezo Na. 20 kinadokeza kuwa uchanganuzi umeongozwa na mkabala (nadharia) wa kimuundo. Hata hivyo, ndani yake kuna istilahi kama vile kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu ambazo ni istilahi za kimuundo. Kwa hiyo, uchanganuzi huo unachanganya mikabala ya kiuchanganuzi.

Kadhalika, katika kitabu cha *Kiswahili-1: Nadharia ya Lugha, Kidato cha Tano, Sita na Elimu ya Juu* (Saluhaya, 2016) kuna uchanganyaji wa vipashio vya kimuundo katika uchanganuzi wa sentensi kwa mkabala wa kimapokeo. Mwandishi wa kitabu alijitanabaisha kuwa kueleza kuwa uchanganuzi unaongozwa na mkabala wa kimapokeo lakini uchanganuzi una viambajengo vya kimuundo 'KN' na 'KT'. Kielelezo Na. 21 kinadhihirisha haya.

**Kielelezo Na. 21: Uchanganyaji wa Vipashio vya Kimuundo Kiuchanganuzi katika Uchanganuzi wa Kimapokeo Saluhaya (2016)**




**Chanzo:** Saluhaya (2016:140)

Istilahi 'K (kiima)' na 'A (kiarifu)' katika Kielelezo Na. 21 zinadokeza kuwa uchanganuzi umeongozwa na mkabala wa kimapokeo. Walakini, katika uchanganuzi huo kuna istilahi, kama vile kirai nomino, kitenzi na kielezi ambazo hutumika katika uchanganuzi wa kimuundo.

*Changamoto za Kimaudhui kutoka kwa Baadhi ya Walimu wa Kiswahili*
Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa baadhi ya walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za sekondari nchini Tanzania wana changamoto za kimaudhui katika uchanganuzi wa sentensi. Katika majibu ya hojaji, baadhi ya walimu walidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusu nadharia (mikabala) ya uchanganuzi wa sentensi. Mara nyingi, ufundishaji wao huongozwa na yale yaliyomo katika vitabu vya kiada na zaida. Maudhui yaliyomo katika vitabu hivyo hufundishwa kama yalivyo kwa wanafunzi wa sekondari. Kutokana na sababu hii, ndiyo maana makosa ya uchanganyaji wa mikabala au vipashio yaliyopo kwenye vitabu vya kiada na ziada hujitokeza kama yalivyo katika uchanganuzi wa wanafunzi.

*Baadhi ya Vipengele Vinavyofundishwa Havimo katika Mihtasari ya Ufundishaji*
Matokeo ya utafiti huu kutoka kwa wanafunzi wa shule za upili wa chini yanaonesha kuwa baadhi ya vipengele wanavyofundishwa havijaelekezwa na muhtasari wa Kiswahili kidato cha I-IV. Kwa mfano, watoataarifa walijibu kuwa njia za uchanganuzi wa sentensi walizojifunza ni majedwali, matawi, maelezo na mishale. Hata hivyo, muhtasari wa Kiswahili kidato cha I-IV unaonesha sentensi zichanganuliwa kwa njia ya matawi na majedwali. Aidha, hatua za uchanganuzi wa sentensi hazijaelekezwa kufundishwa katika muhtasari wa Kiswahili kidato cha I-IV. Walakini, baadhi ya wanafunzi wanataja hatua tano za uchanganuzi wa sentensi (kimapokeo) au nne (kimuundo). Kimapokeo hatu hizo ni kutambua aina ya sentensi, kutaja sehemu kuu za sentensi, yaani kiima na kiarifu, kubainisha vijenzi vya kiima na kiarifu, kutaja maneno yanayounda vijenzi vya kiima na kiarifu na mwisho ni kuandika sentensi upya (TET, 2021). Kimuundo hatua hizo ni kutambua aina ya sentensi, kubainisha vijenzi vikuu, yaani KN na KT, kutaja kategoria za kileksika zinazounda vijenzi vikuu na mwisho kuandika upya sentensi (TET, 2021).

Kwa upande wa shule za upili wa juu, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa wanafunzi wamefundishwa njia tano za uchanganuzi wa sentensi. Njia hizo ni matawi, majedwali, maelezo (vipashio), mishale na mabano. Hata hivyo, muhtasari wa Kiswahili kidato cha V-VI unaonesha kuwa wanafunzi wachanganue sentensi kwa njia tatu ambazo ni majedwali, vipashio (maelezo) na matawi. Aidha, kipengele cha hatua za uchanganuzi wa sentensi hakijaelekezwa kufundishwa lakini mwanafunzi hufundishwa kipengele hicho.

**Mapendekezo ya Utafiti**
Utafiti huu unapendekeza kuwapo kwa mafunzo elekezi kwa waalimu wa sarufi wa shule za sekondari nchini Tanzania. Semina hizi ziongozwe na wabobezi wa masuala ya uchanganuzi wa sentensi ili kuwaongezea maarifa walimu wanaofundisha sarufi katika shule za sekondari. Vilevile, inapendekezwa usasishaji wa vitabu vya kiada na ziada vya somo la Kiswahili katika shule za sekondari. Vitabu hivyo vipitiwe vizuri ili kuondoa matatizo yaliyoelezwa katika makala haya. Kadhalika, miongozo mipya itungwe ili kuonesha baadhi ya mambo ambayo hayapo wazi. Kwa mfano, mkabala wa kiuchanganuzi unaopaswa kutumika katika shule za upili wa chini na wa juu.

Sambamba na hayo, utafiti huu unapendekeza uteuzi wa mkabala mmoja katika shule za upili wa juu na mkabala mwingine katika shule za upili wa chini. Kwa mfano, mkabala wa kimuundo utumike katika shule za upili wa chini ilhali mkabala wa kimapokeo utumike katika shule za upili wa juu. Mapendekezo haya yanakusudia kuondoa tatizo la uchanganyaji wa mikabala na vipashio vyake katika uchanganuzi wa sentensi. Pia, tunapendekeza kuimarishwa kwa ufundishaji wa kozi ya sintaksia ya Kiswahili katika vyuo vikuu ili kutengeneza wahitimu wenye stadi na maarifa mwafaka ya uchanganuzi wa sentensi.

**Hitimisho**
Makala haya yanatoa mchango wa kimaarifa katika sarufi ya lugha ya Kiswahili hasa uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili. Tofauti na watangulizi wetu, kwa mfano Massamba na wenzake (2012), wameonesha kuwa vitabu vya kiada na ziada vina changamoto nyingi kuhusu uchanganuzi wa sentensi. Aidha, utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu matatizo waliyonayo wanafunzi katika uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili. Vilevile, Tafiti za awali (kwa mfano, Kahigi na Hassan (2021) wameonesha kuwa wahitimu wa ualimu katika somo la Kiswahili wanakabiliwa na changamoto ya

kimaudhui kutokana na ufundishaji wa kozi ya sintaksia katika vyuo vikuu vya Tanzania. Utafiti huu unaibua maarifa mapya matatizo waliyonayo wanafunzi wanaofundishwa na walimu waliohitimu mafunzo ya ualimu katika vyuo hivyo.

Pamoja na hayo, utafiti huu haukushughulikia vipengele vyote vya sarufi vinavyofundishwa katika somo la Kiswahili kwa shule za sekondari. Vipo vipengele vingine vinavyofundishwa katika shule za sekondari kama vile mofimu, aina za maneno, ngeli na uambishaji. Utafiti mwingine unaweza kuangazia namna vipengele hivyo vinavyofundishwa katika shule za sekondari nchini Tanzania. Vilevile, uchunguzi mwingine unaweza kufanyika ili kuchunguza matatizo ya uchanganuzi wa sentensi kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya Afrika Mashariki.

**Marejeleo**

Hassan, F. (2021). Mikabala ya Uchanganuzi wa Viambajengo vya Sentensi na Istilahi Zinazotumika: Mifano kutoka Lugha ya Kiswahili. *Mulika*, *40*(2), 1-22.

John, J. (2011). *Kiswahili Kidato cha Tatu: Kitabu cha Mwanafunzi* (Toleo la 2). Dar es Salaam: Oxford University Press Tanzania Ltd.

John, J. na Mduda, F. (2012). *Kiswahili Kitado cha Tano na Sita: Kitabu cha Mwanafunzi*. Dar es Salaam: Oxford University Press (T) Ltd.

Kahigi, K. K. na Hassan, F. (2020). Matatizo ya Ufundishaji wa Sintaksia katika Vyuo Vikuu Nchini Tanzania. *Jarida la Mnyampala*, *1*, 105-120.

Kayne, R. S. (1994). *Antisymmetry in Syntax*. Cambridge MA: The MIT Press.

Lewis, M. (1993). *The Lexical Approach: State of ELT and a Way Forward*. Hove: Language Teaching Publications.

Masebo, J. A. Na Nyangwine, N. C. M. (2016). *Nadharia ya Lugha-Kiswahili 1: Kidato cha 5 na 6*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. na Hokororo, J. I. (2012). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyuo* (Chapa ya Nne). Dar es Salaam: TUKI.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publisher Limited.

Mohamed, A. M. (1986). *Sarufi Mpya*. Dar es Salaam: Dar es Salaam Press and Publicity Centre.

Ndumiwe, E. J. (2020). *Kurunzi ya Isimu na Muundo wa Kiswahili*. Mwanza: Tridax Africa Company Limited.

Ndumiwe, E. J. (2022). Utelezi wa Uainishaji wa Baadhi ya Maneno ya Kiswahili: Kigezo cha Kimofosintaksia. *Jarida la Fahari ya Kiswahili,* 1*(*1), 92 - 104.

Nkwera, F. M. (1978). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Saluhaya, M. C. (2016). *Kiswahili-1: Nadharia ya Lugha, Kidato cha Tano, Sita na Elimu ya Juu*. Dar es Salaam: Ahmadiyya Printing Press.

TET. (1988). *Kiswahili Sekondari*. Dar es Salaam: Short Prints.

TET. (2021). *Kiswahili Shule za Sekondari: Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tatu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (2005). *Muhtasari wa Somo la Kiswahili kwa Elimu ya Sekondari: Kidato cha I-IV*. Dar es Salaam: TET.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (2010). *Muhtasari wa Kiswahili kwa Elimu ya Sekondari: Kidato cha V-VI*. Dar es Salaam: TET.